

# HWDSB

## Orodha ya Kuchunguza COVID-19 kwa Mwanafunzi wa HWDSB

Ijazwe kila siku kabla ya kufika shuleni.

---

**1. Je, mwanafunzi, au mtu yeyote wa kaya yako, ana dalili zozote zifuatazo:**

- Homa (joto la nyuzi 37.8 Celsius/nyuzi 100.4 Fahrenheit, kuhisi joto kwa kumgusa)
- Kikohozi kilichoanza au kinachozidi (kinachoendelea, au kilichozidi kawaida)
- Kupumua kwa shida (kuishiwa na pumzi, kushindwa kupumua kwa undani)
- Hana dalili yoyote kati ya zilizopo hapo juu

**2. Je, mwanafunzi ana dalili zozote zifuatazo:**

- Kikohozi cha kubanja, (kutoa sauti ya filimbi ukipumua)
  - Kuhisi baridi
  - Kuwashwa kwa koo au ugumu wa kumeza
  - kutokwa kwa makamasi, kuziba kwa pua (isiyohusiana na mzio wa msimu au sababu/hali nyingine zinazojulikana)
  - Kupoteza uwezo wa kuhisi ladha au harufu
  - Maumivu ya kichwa yasiyo ya kawaida au ya kudumu kwa muda mrefu
  - Mambo ya mmeng'enyoo wa chakula kama kuhisi kichefuchefu/kutapika, kuendesha, kuumwa tumbo ambako hakuhusiani na sababu au hali zinazojulikana
  - Kuchoka sana ambako sio kwa kawaida (uchovu, kupoteza nguvu)
  - Kuanguka mara kwa mara
  - Maumivu ya misuli yasiyo ya kawaida au ya kudumu kwa muda mrefu
  - Kiwambo
  - Kwa watoto wadogo na wachanga: uvivu au kukosa hamu ya kula
- Hana dalili yoyote kati ya zilizopo hapo juu

**3. Je mwanafunzi alifanya safari ya kimataifa ndani ya siku 14 zilizopita (nje ya Canada)?**

- Ndiyo
- Hapana

**4. Je mwanafunzi alikaribiana na mtu aliyethibitishwa au anayewezekana kuwa ameathiriwa na COVID-19?**

- Ndiyo
- Hapana

# HWDSB

5. Je mwanafunzi alikaribiana na mtu ambaye ni mgonjwa mwenye dalili mpya za kupumua au ambaye alisafiri hivi karibuni nje ya Canada ndani ya siku 14 zilizopita?

- Ndiyo
- Hapana

Ikiwa ulijibu **HAPANA** kwa maswali yote, mwanafunzi amefaulu katika uchunguzi na anaweza kuhudhuria shule leo. Ikiwa wakati wa shule na mwanafunzi anaanza kuhisi vibaya, anapaswa kumwambia mwalimu.

***Ikiwa ulijibu NDIYO kwa maswali yoyote ya uchunguzi, au kama unakataa kujibu maswali, basi mwanafunzi hajafaulu katika uchunguzi na hawezi kuhudhuria shule na anapaswa kuwasiliana na Idara ya Afya ya Umma (905) 974-9848 au daktari wako wa familia ili kupimwa. Tafadhali wasiliana na shule ya mwanafunzi kutoa taarifa ya kutokuwepo kwake. Ikiwa mwanafunzi atapimwa COVID-19, shule itashukuru sana kupata matokeo ya kipimo hicho.***

## Vikumbusho vya Kusaidia Ukiwa Shuleni

- nawa mikono kila mara kwa kutumia maji na sabuni kwa angalau sekunde 20
- tumia kitakasa mikono chenye msingi wa pombe kama maji na sabuni hazipatikani
- jitahidi kutogusa macho yako, pua au mdomo
- dumisha umbali wa kimwili kutoka kwa watu wengine wa angalau mita 2 (futi 6)
- kwa wanafunzi wa darasa la 4 hadi la 12, ni lazima wavae barakoa au kifuniko cha uso (isipokuwa walioruhusiwa na mkuu wa shule)
- wanafunzi wa chekechea hadi darasa la 3 wanashawishiwa kuvaa barakoa au kifuniko cha uso
- kohoa au piga chafya kwenye kiwiko chako na sio mkononi
- ikiwa unaanza kuhisi vibaya, tafadhali mwambie mfanyakazi

*Imesashishwa: Agosti 12, 2020*